MERU UNIVERSITY OF SCIENCE AND TECHNOLOGY

P.O. Box 972-60200 – Meru-Kenya
Tel: +254(0) 799 529 958, +254(0) 799 529 959, + 254 (0) 712 524 293,
Website: info@must.ac.ke Email: info@must.ac.ke

University Examinations 2024/2025

FOURTH YEAR FIRST SEMESTER EXAMINATION FOR THE DEGREE OF BACHELOR OF EDUCATION ARTS

EKI 3401: TEXT: STRUCTURE AND ANALYSIS

TAREHE: JANUARI 2025 **MUDA: MASAA MBILI**

MAAGIZO: JIBU SWALI LA KWANZA KISHA UCHAGUE MENGINE MAWILI

SWALI LA KWANZA (ALAMA 30)

a) Fafanua kwa ufupi dhana zifuatazo:

(i) Udhanilizo (alama 3)

(ii) Uchanganuzi usemi (alama 3)

(b) Eleza tofauti kati ya matini andishi na matini semwa. (alama 6)

(c) (i) Eleza dhana ya kidokezwa. (alama 4)

(ii) Bainisha kidokezwa katika usemi ufuatao:

(i) Katika muktadha wa hospitalini: (alama 2)

"Leo hautarudi nyumbani."

(ii) Katika muktadha wa darasani: (alama 2)

"Mna joto jingi darasani."

(d) *Soma matini ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata:*

Mlahaka wake na wafanyakazi wa kampuni ulikuwa wa kupigiwa mfano. Sasa alikuwa katika hali mahututi. Onyango, daktari alikuwa amesema kuwa hangemtibiwa tena kwa kuwa bima yake ya matibabu haikuwa imelipiwa kwa muda wa miezi kadhaa.

Wakati wa uhitaji wake ndipo aliamua kukata bomba lililomletea maji yaliyomkatia kiu. Kwa nini akate msaada wakati aliuhitaji zaidi, tena kwa dharura. Lisilobidi hubidi. Fatuma, mkewe, aliamua kuuza ng'ombe wao wa mwisho aliyekuwa akikamuliwa lita kumi za maziwa kila siku. Angelivumiliaje kumwona mumewe akigaragara chini kwa uchungu usiomithilika?

(i) Kwa kutoa mifano kutoka kwa matini, eleza dhana ya mrejeleondani na mrejeleonje. (alama 4)

(ii) Eleza mbinu zozote **tatu** alizotumia mwandishi wa matini kuboresha muwala wa matini (alama 6)

SWALI LA PILI (ALAMA 20)

a) Eleza maana ya muktadha katika taaluma ya Uchanganuzi Usemi (alama 4)

b) Fafanua aina NNE za muktadha katika uchanganuzi wa matini ukieleza umuhimu wa kila mojawapo. (alama 16)

SWALI LA TATU (ALAMA 20)

a) Fafanua sifa NNE za matini yenye mshikamano. (alama 4)

b) Kwa kuzingatia kanuni NNe za ushirikiano za Grice, onyesha umuhimu na athari za kuzivunja kanuni hizo. (alama 16)

SWALI LA NNE (ALAMA 20)

a) Taaluma ya Uchanganuzi Usemi ina faida si haba. Jadili (alama 8)

b) Fafanua misingi ya nadharia ya Austin ya Tendo la Usemi ukitumia mifano maridhawa. (alama 12)

SWALI LA TANO (ALAMA 20)

a) Eleza maana ya usemi. (alama 4)

b) Jadili mambo mbalimbali yanayoathiri uteuzi wa usemi (alama 16))